

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI MUHTASARI WA MFUMO WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA JAMII (ESMF) WA UTEKELEZAJI WA MRADI WA TANZANIA YA KIDIJITALI (DTP)

### 1. Maelezo ya Awali

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (WMTH) inaandaa Programu inayopendekezwa ya Tanzania ya Kidijitali (DTP) inayotarajiwa kufadhiliwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB). Lengo la Mradi pendekezwa wa DTP ni kuongeza upatikanaji wa huduma za mtandao wa Intaneti zilizo bora na kwa bei nafuu kwa serikali, wafanyabiashara na raia; na kuboresha uwezo wa Serikali kutoa huduma za umma za dijitali. Mradi wa DTP umebuniwa kufuatia mafanikio yaliyopatikana kupitia Programu ya Miundombinu ya Mawasiliano ya Kikanda – Regional Communication Infrastructure Programm Tanzania (RCIP-TZ).

Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuwa wa awamu mbili kuu kwa kipindi cha miaka mitano kwa kila awamu. Awamu ya I (2021-2025) na Awamu ya Pili (2024-2029) ambazo zitashughulikia vipengele vikuu kama itakavyoelezewa katika taarifa hii. Aidha, miradi midogo midogo itatekelezwa ndani ya kila kipengele kikuu cha mradi. Usimamizi mkuu wa DTP utakuwa chini ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (WMTH) kwa kushirikiana kwa karibu na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB).

Kama sehemu ya maandalizi ya DTP, na kwa kuzingatia utaratibu wa Benki ya Dunia wa usimamizi wa masuala ya Mazingira na Jamii, Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMF) na Mfumo wa Sera ya Uhamishaji wa Makazi (RPF) wa uliokuwa mradi wa RCIP-TZ, umehuishwa na utatumika kwa DTP. Hivyo nyaraka hii ya ESMF iliyohuishwa, inatoa miongozo ya usimamizi, tathmini na upunguzaji wa athari kwa mazingira na jamii ambao unakidhi mahitaji ya kitaifa na ya Benki ya Dunia (kama vile Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (ESIAs) na Mipango ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMPs)). Aidha, RPF iliyohuishwa inalenga kuhakikisha kuwa pale ambapo haiepukiki kuchukuliwa ardhi kwa shughuli za mradi, basi uhamisho wa makazi pamoja na fidia stahiki kwa ardhi iliyopotea, maisha, na mali zingine itapaswa kuzingatiwa na kutekelezwa kwa njia ambayo ni endelevu kama ilivyoinishwa katika ESMF hii.

**Pamoja na nyaraka hii ya ESMF, nyaraka nyingine ambazo zitapaswa kuandaliwa kabla ya tathmini ya mradi ni:**

- Mfumo wa Sera ya Uhamishaji wa Makazi (Resettlement Policy Framework - RPF);
- Mpango wa Kushirikisha Wadau (Stakeholders Engagement Plan - SEP); na

- Mpango wa Ridhaa kwa Mazingira na Jamii (Environmental and Social Commitment Plan - ESCP).

**Pia, nyaraka nyingine ambazo zinapaswa kuandaliwa kabla ya mradi kuanza ni:**

- Mfumo wa Mpango wa Vikundi vilivyoko Pembezoni (Vulnerable Groups Planning Framework - VGPF); na
- Taratibu za Usimamizi wa Kazi (Labour Management Procedures - LMP).

## **2. Vipengele vya Mradi**

**Mradi wa Tanzania ya Kidijitali unachangiwa na vipengele vikuu vitatu kwa ajili ya kuwezesha maendeleo ya kidijitali:** (i) **Ekolojia ya Kidijitali:** Kwa ajili ya kuimarisha sheria, sera, kanuni, uwezo wa kitaasisi na watu unaohitajika kukuza uwekezaji wa miundombinu ya TEHAMA, ushindani wa soko, ushiriki wa kidijitali, kutengeneza ajira na ubunifu; (ii) **Uunganishaji wa kidijitali:** Kwa ajili ya kuhakikisha ufikaji wa huduma za intaneti za bei nafuu, zenye ubora wa hali ya juu kwa raia wote, wakiwemo wa vijijini na kwa taasisi muhimu za serikali; na (iii) **Jukwaa na Huduma za Kidijitali:** Kwa ajili ya kujenga uwezo wa kiufundi, kiutaalam, kitaasisi, na miundombinu ya kidijitali ya serikali kwa ajili ya Serikali kuweza kutoa huduma kwa raia na kufanya shughuli zake kidijitali.

### **Kipengele cha Kwanza: Ekolojia ya Kidijitali.**

Lengo la kipengele hiki ni kuifanya Tanzania kuwa mahali pa kuvutia zaidi na kwenye ushindani katika uwekezaji na ubunifu wa kidijitali, kuhakikisha kuwa faida za teknolojia ya kidijitali inawafikia wananchi wote na hivyo kusaidia kuweka msingi wa ukuaji wa uchumi wa kidijitali. Hili litatimizwa kwa kuimarisha masuala yanayohusiana na mazingira ya kustawisha ekolojia ya kidijitali yaani kwa kutunga na kufuata sheria, kanuni na sera zenye maono ya mbele; kujenga ujuzi na uwezo wa kidijitali wa taasisi na vijana; kuendeleza kundi kubwa la wabunifu, wajasiriamali, na huduma saidizi; kuendeleza tasnia imara ya TEHAMA ya ndani iliyojengeka kwa misingi ya uwekezaji binafsi na yenye uwezo wa kutoa huduma za kufanya biashara kielektroniki, na kuondoa pengo la kidijitali ili kuhakikisha kuwa raia wote na wafanyabiashara wanafuata na maendeleo ya kidijitali. Malengo haya yatatimia kupitia:

#### **(i) Mazingira wezeshi ya kidijitali**

##### **a. Kuanzishwa kwa Kituo cha Kitaifa cha Maendeleo ya Wataalam na Ubunifu wa TEHAMA**

Lengo la shughuli hii ni kuanzisha kituo cha kitaifa cha maendeleo ya wataalam wa TEHAMA na vituo vya teknolojia kwa ajili ya vijana, wajasiriamali na biashara ndogo ndogo na za kati katika maeneo matano ya nchi ili kukuza ubunifu wa ndani nchini. Utekelezaji wa shughuli hii utafanyika kwa kushirikiana na taasisi za elimu ya juu, taasisi za mafunzo ya ufundi, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH). Eneo hili litahitaji ushirikiano wa karibu na sekta binafsi kwa ajili ya kuhakikisha kuwa wataalamu wapya wa TEHAMA waliopewa mafunzo, wanakuwa tayari kuingia kazini wakiwa na sifa na

ustadi unaohitajika kwa kampuni za sekta binafsi, na pia ufahamu wa usalama wa mitandao. Mradi utafuatilia kwa karibu ushiriki wa wanawake katika kunufaika na mafunzo yatakayotolewa, na kukuza mafunzo ya vitendo kwa vijana wa kike chini ya mpango utakaofadhiliwa na Serikali wa ajira kwa vijana. Ushirikiano wa moja kwa moja na sekta binafsi utawekwa, ikiwepo kuwa na programu maalum za kazini au mafunzo yanayotolewa na vituo vya ubunifu(soft centers). Kituo cha kitaifa kitaanzishwa katika ofisi za Tume ya TEHAMA zitakazojengwa Dodoma na vituo vinne vya ubunifu navyo vitaanzishwa katika taasisi za mafunzo au vyuo vikuu. Kimsingi, vituo vya ubunifu vitasambazwa katika maeneo manne kikanda kwa kanda za Kaskazini, Kusini, Pwani na Magharibi. Vigezo vya uteuzi wa vituo na taratibu za uratibu na usaidizi zitaandaliwa na kufafanuliwa katika mwongozo wa utekelezaji wa mradi. Vituo vya ubunifu vitasaidiwa kuandaa njia za urejeshaji wa gharama kutokana na huduma watakazotoa na itahitajika kuanzisha uhusiano mzuri na wateja wa sekta binafsi ili kuwa na uendelevu kwa kipindi kirefu, mara tu fedha za mradi zitakapokwisha.

#### **b. Uanzishwaji wa Maabara ya Matengenezo (Fabrication Labs)**

Shughuli hii inakusudia kuanzisha Maabara ya Matengenezo (FabLabs) kwa ajili ukarabati wa vifaa chakavu vya TEHAMA, na kuhuisha programu tumizi ili viweze kutumika tena kwa kuviongezea muda wa kutumika, na pia kusaidia juhudi za kusambaza vifaa vya TEHAMA kwa taasisi za elimu. Hili litachangia upatikanaji wa vifaa vya TEHAMA vya gharama nafuu kwa madhumuni ya kujifunza. Kwa nyongeza, uanzishwaji wa “FabLabs” hizi utasaidia kupunguza taka zitokanazo na vifaa vya elektroniki (e-waste) na pia kujenga uwezo nchini Tanzania, wa kutumia tena na kuongeza muda wa matumizi kwa vifaa vya TEHAMA. Huu ni mkakati muhimu wa siku zijazo katika kushughulikia taka zitokanazo na vifaa vya elektroniki. Maabara tatu zinataraajiwa kuanzishwa, na vigezo vya uchaguzi wa mahali vitakapoanzishwa vitaelezewa katika mwongozo wa utekelezaji wa mradi. Maabara hizi zitatakiwa kuandaa njia za urejeshaji wa gharama kutokana na huduma watakazotoa na pia njia za kutafuta msaada kutoka kwa sekta binafsi ili kuwa na uendelevu kwa kipindi kirefu, mara tu fedha za mradi zitakapokwisha.

#### **c. Mapitio ya Uthibiti wa TEHAMA**

Chini ya shughuli hii, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Uthibiti wa Mawasiliano (TCRA) na kwa kushauriana na watoa huduma za mawasiliano wenye leseni na kwa msaada wa washauri waelekezi, itafanya mapitio ya mazingira ya kisheria na kisera ili kubaini mapungufu yanayozuia maendeleo ya uchumi wa kidijitali nchini Tanzania. Hii italenga utekelezaji kwenye mkongo wa mawasiliano na kupata mapendekezo kuhusu mipango yoyote mipya inayoweza kuwa muhimu katika kuandaa mazingira wezeshi ya uthibiti, kisheria na kifedha kwa ajili ya Uchumi wa Kidijitali. Katika shughuli hii, Wizara pia itakutana na TCRA na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto ili kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia yanajumuishwa katika mapitio hayo ya udhibiti katika uchumi wa kidijitali. Matokeo ya mapitio hayo yatatumika katika utekelezaji wa mradi kwa ujumla, lakini hasa katika eneo la maunganisho vijijini (rural connectivity). Shughuli

zitakazofadhiliwa katika eneo hili zitajumuisha pia washauri elekezi na gharama mashauriano na wadau.

**(ii) Miundombinu ya kusaidia maendeleo ya TEHAMA Kitaifa na kimataifa na kukuza Biashara za Kielektroniki.**

**a. Kuimarisha mfumo wa kitaifa wa anwani na namba za posta**

Hii ni shughuli inayoendelea ambayo itatanua miradi ya majaribio ya Miundombinu ya Kitaifa ya Takwimu (NSDI). Shughuli hii inasimamiwa na TCRA, ambayo hadi sasa imejumuisha kata 66 (<http://www.address.go.tz/>). Mpango huu unatarajiwa kuhusisha kata 711 zilizopo katika Halmashauri 37 ambazo zinajumuisha Miji Mikuu, maeneo ya mkakati, Wilaya zenye biashara kubwa na maeneo mengine yenye mapato mengi. Shughuli zilizo chini ya mpango huu zitajumuisha utengenezaji wa ramani za kidijitali; barabara na mitaa kupewa majina na uwekaji wa alama na namba za nyumba; ukusanyaji wa taarifa; kuimarisha/kuhuisha kanzidata ya anwani ya taifa; kuandaa/kupitia upya sera na kanuni; kazi za TEHAMA; na uhamasishaji na kujenga uwezo. Ramani ya NSDI, au ramani ya kidijitali, itaweka jukwaa ambalo litakuwa na taarifa zilizopangiliwa kwa ajili ya kusaidia shughuli muhimu kama vile vitambulisho vya taifa vya kidijitali, na ramani za angani kwa ajili ya maendeleo ya taifa. Kazi ya uchoraji ramani itafanywa na maafisa wa serikali na wanafunzi (ambao watapewa malipo ya posho ya kila siku), watakaofanya kazi chini ya uongozi wa Wizara (TCRA na Shirika la Posta Tanzania). Uandaaji wa ramani za chini na upigaji wa picha utasaidiwa na uandaaji wa ramani za kidijitali utakaofanywa na kampuni za kibiashara zitakazo patikana kwa ushindani. Shughuli zitakazo fadhiliwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa, utoaji huduma na kulipia gharama za uendeshaji.

**b. Uendelezaji wa mfumo wa taifa wa usimamizi wa takwimu za TEHAMA**

Shughuli hii inalenga kutoa takwimu za TEHAMA nchini zilizo kamili, sahihi na za wakati kwa ajili ya kusaidia maamuzi ya kisera kwa maendeleo ya taifa. Takwimu hizi zitakusanywa, kwa kufanya tafiti za TEHAMA kwa kaya, kuongezea taarifa kutoka kwenye utafiti uliofanywa mwaka 2017 na Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS). Hili litasaidia ukuaji wa uwekezaji katika sekta ya TEHAMA kwa kutoa taarifa muhimu kwa wawekezaji. Fedha kwa ajili ya eneo hili zitatumika kuwezesha kutengenezwa kwa mfumo wa usimamizi wa kielektroniki, uanzishwaji wa mifumo muhimu ya kuimarisha upatikanaji wa takwimu za TEHAMA na kuchunguza zaidi viashiria muhimu vya TEHAMA chini ya mwongozo wa NBS.

**c. Mipango ya Biashara Mtandao ya Shirika la Posta Tanzania**

Shughuli hii inalenga kusaidia Shirika la Posta Tanzania kuendana na maendeleo ya kiteknolojia ya kisasa na kushiriki kikamilifu katika mpango wa ufanyaji wa Biashara Mtandao (e-Commerce). Mpango huo baadaye utawezesha kujumuishwa kwenye biashara ya kimataifa pamoja na mpango wa Umoja wa Posta (UPU) wa Ecom@Africa. Mpango huo unalenga kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha Biashara ya Kielektroniki katika eneo la Afrika, na itaongeza ukuaji wa biashara na ushiriki wa wananchi katika uchumi wa kidijitali. Shughuli maalum za kipaumbele za hili eneo zimeisha tambuliwa, hata hivyo muundo unaruhusu mradi

kukabili/kushughulikia changamoto mpya na fursa zitakazojitokeza katika sekta hii inayobadilika kwa kasi. Kunaweza kuwepo hitaji la nyongeza ya sheria kwa ajili ya kukuza Biashara Mtandao nchini Tanzania. Hili litashughulikiwa katika kipengele kinachohusu mapitio ya sheria kwenye mradi huu. Fedha zitakazopaswa kulipwa kwenye eneo hili ni kwa ajili ya gharama za washauri elekezi watakaotengeneza jukwaa la Biashara Mtandao.

### **Kipengele cha Pili: Miundombinu ya uunganishaji wa Kidijitali.**

Lengo la Kipengele cha pili ni kuhakikisha kuwa Watanzania wote wanaunganishwa kwenye mtandao wenye kasi kubwa zaidi, kwa bei ya nafuu na wenye kuaminika, ikiwa ni hitaji muhimu la kutoa na kupata huduma za kidijitali kwa maendeleo ya jamii pamoja na ya kiuchumi. Mbali na hatua za kuongeza ushindani katika sekta na uwekezaji wa mitandao ya kibinafsi, kuna haja ya uwekezaji wa moja kwa moja ili kukidhi mahitaji ya serikali ya kuwa na miundombinu ya uunganishwaji na pia kutoa motisha kwa sekta binafsi ili kupunguza pengo la kidijitali katika utoaji wa huduma za mtandao kati ya mijini na vijijini. Kipengele hiki kitasaidia ajenda ya serikali ya ukuzaji wa viwanda na maendeleo sawa kwa wote na kuhakikisha kuwa Watanzania wote, mijini na vijijini, wanapata huduma na fursa sawa za kidijitali. Katika hili, vipengele vidogo viwili, kama inavyoonyeshwa hapa chini vitahusika:

#### **a. Kuimarishwa kwa Maunganisho ya TEHAMA ya Serikali**

Eneo hili linalenga kusaidia kuunganishwa kwenye mkondo wa kasi wa mawasiliano kwa Wizara, Idara na Wakala (MDAs), Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) na Taasisi zingine za Serikali ambazo hazijaunganishwa, au zina changamoto ya kasi kwenye Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (GovNet). Inakusudiwa kuunganisha taasisi zingine 200 zitakazojumuisha Halmashauri, Ofisi za Mkoa, Hospitali za Mikoa, Hospitali za Wilaya; na MDAs zingine kwenye huduma za mtandao zenye ufanisi mzuri. Mradi utawezesha kutanuliwa na kuimarishwa kwa mtandao wa GovNet na pia kuongeza njia ya mkongo wa taifa wa mawasiliano kwenda maeneo yanayohitajika na watoa huduma za mawasiliano.

Aidha, Mradi wa Tanzania ya Kidijitali utagharamia ununuzi wa masafa ya mtandao wa mawasiliano ili kufikia uwezo wa angalau 1.5 Gbps kwa kila eneo kwa muda wa miaka kumi. Uwezo huo utatumiwa na MDAs na LGAs kwa ajili ya utoaji wa huduma za serikali. Ununuzi huo wa masafa unalenga kunufaisha pia makundi ya watumiaji ya vipaumbele ikiwemo shule, vyuo vikuu, hospitali, matumizi ya Serikali n.k. Kwa kusaidia vikundi hivyo kupata masafa hayo kwa bei nafuu, itawawezesha kukuza matumizi yao kulingana na mahitaji yao halisi. Teknolojia iliyopendekezwa kwa ajili ya kuunganisha taasisi za serikali itakuwa “fiber optic cable”, lakini pale ambapo haitapatikana, suluhisho la muda kwa kutumia microwave, setilaiti au “4G mobile broadband” inaweza kufikiriwa.

#### **b. Mtandao wa kasi vijijini kwa ajili ya maendeleo**

Sehemu hii inalenga kuendeleza mpango uliofanikiwa wa uunganishaji vijijini uliofanyika chini ya mradi wa RCIP-TZ kwa kutanua ufikaji wa mtandao unaopitisha data (4G au zaidi) kwenda kwa zaidi ya watu milioni tatu wanaoishi katika maeneo ya nchi ambayo kwa sasa hayafikiki na mitandao yoyote na pia

kuboresha mitandao iliyopo ya 2G kuwa 4G au zaidi. Hii itahimiza ushiriki katika maendeleo ya uchumi wa kidijitali na itasaidia maeneo ya vijijini ambayo hapo awali hayakuweza kushiriki katika mafunzo ya mtandaoni au kushiriki kwa mikutano ya mbali, kufanya hivyo. Programu hii itatekelezwa kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na uzoefu kutoka kwa programu ya RCIP-TZ utatumika, kwa mfano kurekebisha njia za utoaji wa vivutio vya kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika maeneo ya vijijini kwa kutumia mtandao wa kuzunguka (network roaming). Eneo hili pia litashughulika na "TV white spaces", masafa yaliyokuwa yanatumika kwa ajili ya runinga za analojia ambayo sasa hivi hayatumiki. Hili litahitaji utafiti wa mshauri elekezi kwa kufanya uchambuzi kamili ili kuona upeo wa kutumia wigo wa "TV white spaces" katika maeneo ya vijijini na hivyo kutoa mwongozo wa sera na udhibiti juu ya utumiaji wa fursa hii.

Shughuli zinazofadhiliwa eneo hili ni pamoja na a) utafiti juu ya upeo wa kutumia wigo wa "TV white spaces"; b) utafiti juu ya namna gani minada ya kuwapata watakaopewa ruzuku itakavyoendesha; c) minada ya ruzuku, iliyo wazi kupitia zabuni za ushindani, katika maeneo yaliyobainishwa na UCSAF. Washindi wa zabuni chini ya mradi huo watalazimika kufuata viwango husika vya usimamizi wa mazingira na jamii kwakazi yoyote ya ujenzi itakayofanyika (kwa mfano, ujenzi wa minara ya simu).

### **Kipengele cha Tatu: Jukwaa la Huduma za Kidijitali**

Lengo la kipengele hiki ni kuongeza uwezo wa miundombinu ya msingi inayohitajika katika utoaji wa huduma za umma za kidijitali, kuongeza ufanisi wa shughuli za ndani za serikali na kuendeleza majukwaa ya uzalishaji wa huduma za umma za kidijitali zenye vipaumbele katika kukuza uchumi na kuendeleza sekta. Kuna maendeleo yaliyofanyika katika miaka ya hivi karibuni katika kukuza huduma za kidijitali na majukwaa shirikishi ya kutolea huduma ('mobile services portal', 'SMS gateway', 'e-payment gateway', n.k.); kuimarishwa kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) na kuweka mifumo ya uzalishaji ya kidijitali ya Serikali (awamu ya kwanza ya Ofisi Mtandao, Mfumo wa kidijitali wa kumbukumbu, mfumo wa usimamizi wa mapato, n.k.). Hivyo basi kutokana na umuhimu wa Mifumo hii, serikali inalenga kuendelea na utekelezaji wa Mifumo mbalimbali kwa ajili ya kuleta huduma karibu kwa wananchi na kukuza uchumi wa kidijitali kwa kutoa fursa zaidi kwa kila mwananchi kushiriki kwenye kujenga uchumi. Kipengele hiki kitatekelezwa kupitia maeneo yafuatayo:

#### **(i) Huduma za Kidijitali na Mifumo ya Uzalishaji**

##### **a. Vituo vya Kutolea Huduma Sehemu Moja (Huduma Jamii Centres)**

Shughuli hii inalenga kuboresha michakato na taratibu zilizopo za utoaji huduma za serikali kwa raia na wafanyabiashara ndogondogo kwa kuanzisha Vituo 31 vya kutoa huduma sehemu moja (One Stop Service Centers - OSSC, au Huduma Jamii kwa Kiswahili), ambapo hadi vituo 10 vitatekelezwa katika miaka miwili ya mradi (8 bara na 2 Zanzibar) Vituo hivi vitatengenezwa na kuwezesha raia kupata huduma za umma kwa njia rahisi, ya haraka na isiyo na vikwazo katika sehemu moja ambayo ni rahisi kwa usimamizi, kwa mfano ofisi za posta, vituo vya kijamii

au mjasiliamali wa ndani. Upembuzi Yakinifu ulikamilishwa mnamo Novemba 2020, na mapendekezo ya utekelezaji wa shughuli na maeneo ya OSSCs yalitolewa. Mwisho wa mradi, imepangwa kuwa hadi huduma 32 za Serikali zitatolewa. Upembuzi Yakinifu umependekeza kutumia ada ya utoaji huduma (chini ya asilimia 5 ya gharama ya huduma uliyopewa) kama njia ya kufadhili OSSC.

Sambamba na rasimu ya bajeti iliyowasilishwa katika upembuzi yakinifu, shughuli zitakazofadhiliwa katika eneo hilo zitajumuisha ada za mshauri elekezi kwa ajili ya uboreshaji wa mchakato wa biashara. Shughuli zingine zinazofadhiliwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA na ukarabati wa majengo yaliyopo. Mafunzo ya wafanyikazi wa utendaji pia yatahitajika, hasa kwa uelewa wa usalama wa kimtandao. Mradi utatumia majengo ya serikali yaliyopo na kazi zozote za ujenzi zitazingatia matakwa ya uhifadhi wa mazingira na jamii ya nchi na Benki ya Dunia.

#### **b. Uchumi wa Kidijitali**

Shughuli hii, itakayotekelezwa chini ya Wizara ya Fedha na Mipango na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), itazingatia uboreshaji wa mifumo ya kifedha/malipo kwa kuimarisha kanuni zinazohusu shughuli za kifedha za dijitali, kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), na kuimarisha Mfumo wa Malipo wa Kitaifa (NPS). Kwa kuweka taratibu na mifumo itakayosimamia vyema uchumi wa kidijitali. Shughuli hii inapaswa kuchangia ongezeko la mapato kwa Serikali. Shughuli hii itahitaji huduma za washauri elekezi, ununuzi wa vifaa na huduma za TEHAMA, pamoja na utengenezaji wa programu na ushauri wa usalama wa mitandao.

#### **(ii) Miundombinu ya Kuhifadhi Data**

Shughuli hii inakusudia kuimarisha Miundombinu ya Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data kwa kupata vifaa vya kuhifadhia, vifaa vya mitandao, na rasilimali za kompyuta kwa ajili ya jukwaa shirikishi la serikali. Pia inalenga kusaidia kuwezesha matumizi ya pamoja (shared) ya rasilimali kwa gharama nafuu, kuimarisha uhakika wa huduma za kielektroniki zinazotolewa na serikali na kuongeza uwezo wa kuhifadhi data za serikali. Shughuli hii itahitaji huduma za washauri elekezi, ununuzi wa vifaa na huduma za TEHAMA na mafunzo ya ziada, hasa katika eneo la usalama wa mitandao, kwa kuzingatia njia bora za matumizi ya nishati mbadala. Kutokana na unyeti na usiri wa data za serikali, uhifadhi wa data hizo kwenye kituo cha serikali kunahitajika. Kwa ajili hiyo basi, kituo cha data cha serikali, kilichopo ambacho kiliishajengwa, kitatumika na kuimarishwa kwa usalama zaidi na kuongezewa uwezo wa kuhifadhi data.

#### **(iii) Uelewa na Kujenga uwezo katika masuala ya Kidijitali**

##### **a. Programu ya mafunzo ya Kada ya TEHAMA ya Serikalini**

Shughuli hii inalenga kuwajengea uwezo wataalamu wa TEHAMA ndani ya Serikali ili wawe mahiri katika kusimamia na kuhudumia mifumo ya TEHAMA ya serikali iliyopo na inayotarajiwa kuwepo baadaye. Hii inafuatia matokeo ya tathmini ya mapungufu ya ujuzi na taaluma za TEHAMA liliyofanywa katika Wizara zote mwaka 2018. Mradi unalenga kuwapa mafunzo maalum wataalam wa TEHAMA

wasiopungua 500 kutoka Wizara mbalimbali na pia itajumuisha kozi ndefu (digrii za uzamili) katika vyuo vikuu vya viwango vya juu. Ushirikiano utaimarishwa na Kituo cha Kitaifa cha Maendeleo ya Wataalam wa TEHAMA ili kuhakikisha kuwa programu zifaazo zinaandaliwa kwa ajili ya kusaidia wataalamu wa TEHAMA katika sekta ya umma au kwa wale wanaotaka kufanya kazi za serikali. Watumishi wa umma watakao nufaika na mafunzo nje ya nchi watatakiwa kuwa wamefanya kazi serikalini kwa miaka kadhaa na watasaini mikataba ya kukaa ndani ya serikali kwa muda fulani au kujitolea kulipa sehemu ya gharama za mafunzo. Utaratibu wa uteuzi utaandaliwa na kujumuishwa katika Mwongozo wa Utekelezaji wa Mradi (PIM).

#### **b. Elimu ya Kidijitali kwa Umma**

Hii ni programu ya utoaji elimu kwa umma inayolenga kuongeza kiwango cha matumizi ya huduma za serikali za mtandaoni na itakuwa endelevu kwa muda wote wa utekelezaji wa mradi wa Tanzania ya Kidijitali. Itajumuisha, mitandao ya kijamii, vipindi vya runinga na redio kwa ajili ya kutangaza huduma za Serikali; matangazo ya runinga na video fupi fupi; machapisho ya matangazo kwenye vyombo vya habari; usambazaji wa matangazo; na warsha na semina (kwa vyombo vya habari na umma). Shughuli zingine ambazo zitagharimiwa ni pamoja na vikao kwa njia za kidijitali, makongamano, maonyesho na mashindano tofauti ya kidijitali baina ya vijana ili kuimarisha ushiriki wa kidijitali na michango katika ubunifu. Shughuli hiyo inakusudia kuongeza uelewa wa masuala ya kidijitali kwa kuongeza ufahamu na utumiaji wa huduma za kidijitali kwa raia. Aidha, kwa kupitia mashauriano maalum kati ya Serikali na wadau, itahakikishwa kuwa ushiriki wa wanawake katika kupata huduma za raia umezingatiwa. Shughuli zitakazo gharimiwa eneo hili ni pamoja na warsha, huduma za washauri elekezi na mafunzo.

#### **Kipengele cha nne: Usimamizi wa Mradi**

Sehemu hii itasaidia maeneo muhimu ya usimamizi wa mradi, ikiwemo gharama za watumishi na gharama za uendeshaji. Serikali, kupitia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, itaanzisha Kitengo cha Usimamizi wa Utekelezaji wa Mradi (PIU) ambacho kitakuwa na jukumu la kusimamia shughuli zote za mradi. PIU itajumuisha mratibu mkuu wa mradi, mtaalam wa huduma za serikali ya kidijitali, mtaalam wa kiufundi wa TEHAMA na wataalam wa ununuzi na usimamizi wa fedha na pia wataalamu wa masuala ya mazingira na jamii. Eneo hili pia litahusisha gharama za usimamizi wa mawasiliano, ufuatiliaji na tathmini, ukaguzi wa ndani, uendeshaji wa shughuli mbali mbali za kuwezesha mradi na usimamizi wa anuai za jamii. Zaidi ya hayo itajumuisha kujenga uwezo kwa taasisi zinazonufaika moja kwa moja na mradi, kama vile UCSAF na eGA hasa kwenye maeneo ya uandaaji wa nyaraka za zabuni na usimamizi wa mikataba ya TEHAMA.



### **Kipengele cha tano: Kukabiliana na Dharura.**

Mradi unahusisha kipengele cha kukabiliana na dharula. Kipengele hiki hakijatengewa fedha zozote kwa sasa lakini kinaweza kufadhiliwa wakati mradi unaendelea ili kuruhusu kukabili dharura zitakazo jitokeza wakati wa utekelezaji wa Mradi. Kuwepo kwa kipengele hiki katika hatua za mwanzo za maandalizi ya mradi inasaidia kuweka utayari wa kukabiliana na dharula pale inapoibuka. Dharula hizi zinaweza zikawa kwa mfano, majanga ya kibinadamu ambayo yanahitaji utoaji wa huduma za mawasiliano ya dharura ili kuchukua nafasi ya vifaa ambavyo vimeharibiwa, au kuwezesha malipo ya fedha ya dharura kupitia mitandao. Suala la msingi wakati wa andiko hili ni janga la Corona (COVID-19) ambalo linahitaji majibu ya haraka, kwa mfano kwa kuongeza njia na uwezo wa ziada wa mtandao kwa ajili ya ofisi za Serikali, hasa vituo vya afya na hospitali, na kwa watumishi wa Serikali wanaolazimika kufanya kazi wakiwa nyumbani. Mazingira, mawanda na taratibu za ushughulikaji wa masuala ya dharula yatafafanuliwa katika Mwongozo wa Utekelezaji wa Mradi (PIM).

### **3. Shughuli za Mradi na Uhifadhi**

Mradi wa DTP utahusisha miradi midogo midogo ambayo inaweza kuleta athari mbaya kwenye mazingira na jamii. Hata hivyo hali halisi, mahali ilipo, maeneo makuu yenye athari, kiwango, ukubwa, na muda wa athari zitakazotokana na miradi itakayotekelezwa bado hazijabainishwa kwa kina ili kuwezesha tathmini ya athari kwenye Mazingira na Jamii (ESIA) au na maandalizi ya Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMP) kuweza kufanyika na kuidhinishwa kwa kufuata kanuni za nchi.

Sera za Benki ya Dunia za Uhifadhi wa Mazingira zinaweka mahitaji ya tathmini kabla ya kutolewa kwa idhini ya ufadhili. Sera kuu mbili za uhifadhi za Benki ya Dunia zilizoguswa na DTP ni OP 4.01, ya Tathmini ya Mazingira na OP 4.12, kwa ajili ya Uhamisho usio wa Hiari. Kwa hali hiyo basi, ESMF hii inaweka utaratibu wa kufanyika tathmini katika mazingira na jamii kwa ujumla. Aidha inakusudia kuweka vigezo vya kufuatwa kupitia ESIA na ESMPs ili kuhakikisha kuwa majukumu ya Kitaifa na Sera za Benki ya Dunia za uhifadhi zinazotokana na utekelezaji wa DTP zinashughulikiwa.

Aidha, sambamba na sheria zinazotumika Tanzania, ESMF inaweka taratibu na miongozo ya mipango ya mazingira na jamii, uhakiki, uidhinishaji na utekelezaji wa shughuli zitakazofanyika kwenye mradi wa DTP. Vilevile kutambua nafasi, majukumu na kuainisha mahitaji ya uwezo wa utekelezaji kikamilifu wa sheria mbali mbali juu ya mazingira na jamii. Ili shughuli zote zinazohusiana na mradi na uhifadhi ziweze kufanyika vyema, uzoefu wa mazingira, jamii, na mafunzo yaliyopatikana kwenye utekelezaji wa mradi wa RCIP-TZ yanazingatiwa kikamilifu katika ESMF hii ya DTP.

### **4. Athari za jumla za Mazingira na Jamii kwenye mradi wa DTP**

Utekelezaji wa mradi wa DTP utaweza kuleta athari chanya na hasi kama ifuatavyo:

**a. Athari za kiasilia:**

- usumbufu wa maeneo yaliyohifadhiwa;
- mabadiliko ya makazi ya ardhini na majini;
- usumbufu wa uhamaji wa ndege, majeraha na / au vifo;
- athari za radi;
- athari za mazingira na maono;
- uzalishaji wa hewa;
- taka za kielektroniki;
- uchafuzi, na kelele na mitetemo;
- umeme na uwanja wa sumaku;
- uchafuzi wa maji (rasilimali za maji na udongo) kutokana na kumwagika, kuvujishwa, na mafuta kufunguliwa kwa bahati mbaya; na
- ongezeko la matumizi ya nishati.

**b. Athari za kijamii na kiuchumi zinazoweza kutokea:**

- usumbufu kwa jamii za wenyeji;
- kuhamishwa kwa jamii / au kiuchumi kutokana na mabadiliko ya matumizi ya ardhi;
- athari na / au usumbufu kwenye maeneo ya kitamaduni na akiolojia;
- hofu ya usalama kwa umma;
- hofu ya usalama wa afya kazini; na
- usalama kwenye ndege.

**c. Athari Chanya**

- fursa za ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja na fursa za biashara kwa wakazi wote wa vijijini na mijini;
- kuinuka kiuchumi na kimaisha kutokana ukuaji salama wa uchumi;
- kuboresha utoaji wa huduma kwa umma kwa ufanisi kutokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya TEHAMA na kuunganishwa kwa taasisi za serikali;
- ongezeko la maunganisho na upatikanaji wa huduma za TEHAMA vijijini na mijini;
- matumizi ya minara kwa pamoja inayoleta faida ya bei na huduma kwa wateja kupitia ushindani, tofauti na huduma zingine za umma;
- kujenga uwezo na kukuza ujuzi;

- kutanuka kijiografia, kijamii na kiuchumi kwa huduma za sauti au data; na
- kupungua kwa gharama za kupata huduma mbali mbali za umma kwa kutumia TEHAMA.

Kwa nyongeza, ujumuishaji wa uboreshaji wa mazingira katika muundo wa mradi wa DTP pia unaleta faida kwenye mazingira. Uboreshaji na faida zinaweza kuwa:

- kuongezeka kwa uchakataji wa taka;
- kupunguza uzalishaji wa kaboni kwa kuepusha safari zisizo za lazima kwa mikutano na shughuli zingine kwa kutumia vyombo vya moto;
- uwekezaji katika teknolojia mpya ambayo haina vifaa vya hatari; na
- kujali mazingira kwa njia endelevu wakati wa matumizi ya vifaa vya ndani.

## **5. Ushirikishwaji wa Wadau**

Wakati wa uandaaji wa ESMF hii, Mshauri Mwelekezi aliweza kushirikisha kikamilifu wadau na watekelezaji muhimu watakaohusika moja kwa moja na mradi wa DTP. Pamoja na kuwa mradi wa DTP unatarajiwa kutekelezwa katika ngazi zote za kitaifa hadi kwenye halmashauri, mashauriano na wadau hao yalifanywa Dar es Salaam na Dodoma pekee, kutokana na kuwa na muda mdogo wa kufanya zoezi hilo, Mashauriano hayo yalifanywa na Taasisi za Umma na binafsi zinazohusika na utekelezaji, uratibu, na uendeshaji katika ngazi ya kitaifa.

Wadau wakuu waliyoshirikishwa ni pamoja na:

### (i) Wizara

- Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI);
- Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB);
- Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira (VPO-DoE);
- Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (WMTH);
- Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (WVBU);
- Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WEST); na
- Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (WANMM).

### (ii) Wakala za Serikali/au Mamlaka

- Tume ya TEHAMA (ICTC);
- Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF);
- Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA);
- Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL);
- Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA);

- Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA);
- Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA);
- Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA); na
- Shirika la Posta Tanzania (TPC).

(iii) Mdhibiti wa Mazingira

- Baraza la Taifa la Menejimenti ya Mazingira. (NEMC);

(iv) Vyuo vya elimu ya juu

- Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM);
- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM); and
- Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam Institute of (DIT)

(v) Hospitali ya Taifa

- Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)

(vi) Kampuni binafsi za mitandao

- Vodacom, Airtel, Tigo/MIC, and Halotel

(vii) Wafanyabiashara wa taka za kielektroniki waliosajiliwa

Chilambo General Trade Company Ltd

## **6. Hoja muhimu za wadau**

Kwa ujumla, wadau wana mtazamo mzuri kwa mradi wa DTP na wameahidi kusaidia maendeleo na utekelezaji wa programu hiyo. Hata hivyo, hoja zao kuu zilizotolewa wakati wa mikutano ya mashauriano ni pamoja na:

- utoaji wa vibali kwa wakati unaofaa;
- kuingizwa kwa mafunzo yaliyofanyika kwenye mradi wa RCIP-TZ;
- ujenzi wa miundombinu inayosaidia;
- uchukuaji wa ardhi / ununuzi na njia za kufidia;
- uzalishaji wa taka zinazotokana shughuli za ki-elektroniki na usimamizi wake;
- ushiriki wa wadau na kutoa uelewa;
- uendelevu wa mradi;
- uboreshaji wa huduma na mawasiliano ya serikali;
- TEHAMA na viwanda;
- uchafuzi wa mazingira (hewa na ardhi); na
- Hatari za kiafya na usalama sehemu ya kazi.

## **7. Nyenzo za Usimamizi wa Mazingira na Jamii**

Ili kuhakikisha kuwa miradi midogo iliyopangwa kutekelezwa kwenye mradi wa DTP ina utayari wa kukabili athari, mtekelezaji husika atatumia nyenzo zifuatazo:

- Uchunguzi wa Mazingira na Jamii: Miradi midogo midogo inayopendekezwa kwenye mradi wa DTP na shughuli zinazohusiana ziwekwe kwenye mchakato wa kuchunguzwa.
- Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (ESIAs);
- Mipango ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMPs); na
- Tathmini na Ufuatiliaji na Ukaguzi.

Mtekelezaji wa mradi atatumia nyenzo hizi kwa athari zilizopo na zinazotarajia kutokea wakati wa utekelezaji lakini pia nyenzo hizo zitatumika kwa ajili kuhakikisha kuwa mahitaji kwa ajili ya kupata kibali cha mazingira kitaifa yanatekelezwa. Vilevile, nyenzo hizi zitatumika ili kuhakikisha kuwa hoja za mazingira na jamii zimejumuishwa katika mchakato mzima wa kufanya maamuzi na kuleta matokeo ya mradi yanayokubalika katika nyanja zote. Nyenzo hizi zinaelezewa kwa undani kama ifuatavyo:

### **a. Kuchunguzwa kwa shughuli za miradi midogo midogo**

Kitengo cha Usimamizi wa Mradi (PIU) / mtekelezaji wa moja kwa moja (Mteja) atafanya uchunguzi wa awali kwa mradi mdogo uliopendekezwa ili kuweza kuamua juu ya hatua ya athari za mazingira na kijamii itakayochukuliwa kwa kuzingatia mahitaji ya sheria za nchi (Taz. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 Kanuni za EIA na Ukaguzi, 2005). Mara baada ya shughuli ndogo ya mradi kufafanuliwa na eneo kuchaguliwa, mteja atakamilisha andiko la mradi na / au maelezo ya muundo wa awali na kujaza Fomu ya Uchunguzi.

Fomu hiyo itawezesha utambuzi wa athari za mazingira na kijamii zinahusiana na shughuli inayopendekezwa kufanyika. Kwa kuwa ESMF na RPF zitatumika kwa pamoja, basi fomu ya uchunguzi itawezesha utambuzi na tathmini ya athari zitakazohusisha uwezekano wa upatikanaji wa ardhi na uhamisho kwenda makazi mapya bila hiari.

### **b. Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (ESIAs)**

*Kwa Kundi A miradi midogo inayohitaji EIA:*

Mteja atawasilisha nakala ya Taarifa ya Athari za Mazingira (EIS) kwa mamlaka husika (hiyo ni NEMC) ili ikaguliwe. EIS inapaswa kujumuisha taarifa zote muhimu kulingana na kanuni za EIA na Ukaguzi za Tanzania. Kwa miradi midogo ambayo inaweza kusababisha uhamisho kwenda makazi mapya bila hiari, mteja pia atahitajika kuwasilisha Mpango wa Utekelezaji wa Uhamisho wa Makazi (RAP) kwa mamlaka husika ili iidhinishwe. Hili limeelezewa kwa undani zaidi katika RPF ya mradi wa DTP iliyoandaliwa kuambatana na ESMF hii.

### **c. Mpango wa usimamizi wa mazingira na jamii (ESMPs)**

*Kwa Kundi B miradi midogo inayohitaji ESMP:*

Mteja atawasilisha nakala ya ESMP kwa mamlaka zinazohusika na mazingira na kwa wasimamizi wa utekelezaji wa mradi (MWTCs na PO-PSMGG) na Benki ya Dunia. Lengo la ESMP ni kushughilikia mahitaji ya mazingira na jamii yanayohusiana na mradi kwa njia rahisi, yenye majibu, na ya gharama nafuu bila kuzorotesha mwenendo wa mradi. ESMP / EMP inapaswa kuelezea hatua zinazohitajika kwa ajili ya kushughulikia masuala yaliyoibuliwa wakati wa utafiti wa EIA. Aidha, ESMP nzuri inapaswa kuonyesha kuwa shughuli za ufuatiliaji zilizopendekezwa zinajumuisha athari zote kuu na kutambua namna zitakavyo jumuishwa katika usimamizi wa mradi. Hivyo basi ESMP / EMP, inapaswa kushughulikia masuala yafuatayo ikiwa ni kiwango cha chini kwa ajili ya miradi inayohitaji idhini ya ESMP:

- Hatua kuu za kupunguza athari za mazingira na kijamii;
- Programu ya mafunzo na kujenga uwezo kuhusiana na mazingira; na
- Programu ya ufuatiliaji mazingira na jamii.

ESMP / EMP inapaswa kujumuisha yafuatayo:

- Athari zinazoweza kutokea kwa mazingira, jamii, kiafya na usalama zinazohusiana na eneo, ujenzi, na kazi za mradi mdogo;
- Hatua za kupunguza na kufuatilia ushughulikiaji wa athari zinazoweza kujitokeza;
- Wajibu wa kufuatilia mahitaji ya EMP;
- Mahitaji ya mafunzo na ya kujengea uwezo kwa maafisa wa mradi na jamii; na
- Makadirio ya bajeti.

### **d. Tathmini na Ufuatiliaji na Ukaguzi.**

Ufuatiliaji na Tathmini (M&E) ya ESMF ni sehemu muhimu ya mpango wa jumla wa M&E ulioandaliwa kwa ajili ya mradi wa DTP. Mpango wa jumla Ufuatiliaji na Tathmini ulioandaliwa kwa ajili ya mradi wa DTP utajumuisha viashiria vya ufuatiliaji wa athari na kutathmini matokeo dhidi ya malengo ya mradi. Aidha, Ufuatiliaji na Tathmini wa miradi mingine utafanywa na wafanyikazi wa Kitengo cha Usimamizi wa Miradi au Washauri Elekezi. Taasisi zinazohusika na utekelezaji wa moja kwa moja zina jukumu la kusimamia na kutathimini shughuli zao kama ilivyoainishwa katika mradi wa Tanzania ya Kijiditali.

Hivyo, kila mtekelezaji wa mradi mdogo atafanya ufuatiliaji na tathmini katika shughuli zake na pia kuhakikisha kuwa masuala ya ufuatiliaji wa athari na usimamizi yanazingatiwa na kufuatwa kama ilivyoelekezwa katika ESMP na ESIA. Hata hivyo, Ufuatiliaji na Tathmini ya miradi midogo na shughuli zinazohusiana zitafanywa mara kwa mara, angalau mara mbili kwa mwaka, na ripoti ya mwaka itawasilishwa kwa WMTH, OR-MUUUB na Benki ya Dunia. Kwa kutegemea hali ya shughuli za mradi na upatikanaji wa fedha, na hitaji la ufuatiliaji wa karibu, ziara

za ufuatiliaji za mara kwa mara zinaweza kufanywa kwa miradi inayoonyesha dalili za hatari au athari mbaya.

Ili kufanikisha mpango mzuri wa utekelezaji, Kitengo cha Usimamizi wa mradi kwa kushirikiana na watekelezaji wa moja kwa moja wa mradi itaandaa hadidu za rejea , gharama na itajumuisha Ufuatiliaji na Tathmini kwa tafiti zozote za ziada au tathmini zilizopendekezwa kabla ya kufanya ESIA na au ESMP.

## **8. Mahitaji ya Uwezo wa kutekeleza ESMF**

Uzoefu kutokana na mradi uliopita wa RCIP-TZ unaonyesha kuwa kuna haja ya kuhakikisha kuwa uwezo wa kutosha unajengwa kwa ajili ya kutekeleza na kufuatilia utendaji wa ESMF (na RPF) kwa mradi wa Tanzania ya Kijiditali. Kwa kuzingatia hayo, yafuatayo yanapendekezwa:

- i. WMTM kumwajiri Mtaalam wa Mazingira kwa mkataba wa Muda mfupi na pindi hitaji litakapojikiza kama sehemu ya mradi wa Tanzania ya Kijiditali. Mtaalam huyo ataripoti kwa wasimamizi wa utekelezaji wa Mradi. Ili kuchangia katika kutimiza malengo ya mradi, Mtaalam huyo atakuwa na majukumu yafuatayo:
  - Kwa kushirikiana na watekelezaji wa mradi Mtaalam ataandaa mpango kazi wa mwaka na bajeti ya matumizi;
  - Kufuatilia maendeleo ya mradi kuangalia kama inafuata miongozo ya ESMF, kutatua vikwazo vya utekelezaji, na kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mradi wote unaendelea vizuri;
  - Kukusanya na kusimamia taarifa zinazohusiana na mradi na ukaguzi (mfano usimamisi wa mazingira na taarifa za ukaguzi); na
  - Kuhakikisha kuwa vyombo vya utekelezaji vinasaidiwa vya kutosha na kwamba vinazingatia kanuni za mradi na kufuata mahitaji maalum ya ESMF.
- ii. WMTM inapaswa kufanya Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo (TNA) na kuandaa mpango wa mafunzo ili kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa mradi wa DTP katika kila taasisi / wakala na washirika waa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mradi. Kipaumbele cha Mahitaji ya Mafunzo kinapaswa kuwekwa kwa Wataalam wote wa Mazingira / Watu Maalum ambao watahusika na / au kuwa na majukumu katika utekelezaji wa miradi ndogo ya Tanzania ya Kijiditali, haswa kwa ESIA na au ESMPs. Suala hili linahitaji wa lazima katika mpango wa jumla wa kujenga uwezo wa mradi wa Tanzania ya Kijiditali.
- iii. Wataalam wa Mazingira / Watu Maalum kutoka kwa watekelezaji wa mradi wanapaswa kupewa mafunzo juu ya utekelezaji na ufuatiliaji wa ESMF. Mafunzo haya yatahakikisha kuwa wataalamu wanakuwa na uwezo wa kusimamia na kufuatilia mazingira, jamii, Afya na Usalama kwa shughuli za miradi midogo midogo ya Tanzania ya Kijiditali.

- iv. WMTH inapaswa kuzingatia kuwa na mfuatiliaji wa akiolojia atakayekuwa anaitwa mara moja moja "on-call basis" ambaye atashauri juu ya masuala mengine yoyote yanayohusiana na urithi wa kitamaduni yatakayojitokeza wakati wa utekelezaji wa shughuli chini ya mradi wa DTP.